



TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro imepokea fedha katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/19 kugharamia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Njia ya ununuzi itakayotumika wakati wa ujenzi ni **"Force Account"** kwa kuzingatia maelekezo ya matumizi ya njia kwa mujibu wa kanuni na. 167 ya kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016.

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Ngorongoro chini ya sheria ya manunuzi ya Umma na. 7 ya Mwaka 2011 kanuni na. 181 anawatangazia Wananchi, Makampuni na Taasisi mbalimbali kuomba kazi za ufundi katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Kijiji cha **Lopolun** kwa majengo yafuatayo:

1. Jengo la utawala
2. Jengo la wagonjwa wa nje
3. Stoo ya dawa
4. Jengo la maabara
5. Jengo la vipimo vya mionzi (X-Ray)
6. Jengo la kufulia nguo (laundry)
7. Jengo la wazazi

Masharti muhimu ya zabuni

1. Awe raia wa Tanzania
2. Waombaji wawe wamesajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
3. Awe na cheti cha ufundi wa kazi husika kutoka VETA au Taasisi zingine zinazotambuliwa na Serikali
4. Muombaji aweze kutoa risiti ya EFD na risiti ya kukiri mapokezi
5. Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro hailazimiki kukubali kima cha juu wala cha chini cha bei ya mzabuni.
6. Waombaji wawe na leseni na uzoefu wa miaka mitatu (3) au Zaidi.
7. Mwombaji awe na uwezo au uzoefu wa kusoma ramani/michoro.
8. Mwombaji aambatishe udhibitisho wa uzoefu aliyonayo.
9. Ada ya maombi ni Tsh. 50,000/= ambazo hazitarudishwa/rejeshwa
10. Mwombaji aoneshe bei ya kujenga jengo husika.
11. Mwombaji haruhusiwi kuomba jengo Zaidi ya moja.
12. Vitabu vya zabuni vinapatikana katika ofisi ya katibu wa bodi ya zabuni, Halmashauri ya wilaya Ngorongoro, S.L.P 1, Loliondo.
13. Maombi yanatakiwa kufungwa kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na kuonesha aina ya zabuni inayoombwa bila kuwa na viashiria vyovyote inakotoka na yatumwe kwa anuani ifuatayo:

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO,
S.L.P 1,
LOLIONDO.**

N.B

Ramani/mchoro na nukuu za gharama ya ujenzi zinapatikana Ofisi ya Manunuzi(W). muda na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 17/01/2019 saa 4:00 asubuhi na zabuni zitafunguliwa saa 4:30 kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro. Waombaji au wawakilishi wanaruhusiwa kuhudhuria kwenye ufunguzi.

**Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri (W) Ngorongoro**